**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA IRINGA**

**SHULE YA SEKONDARI TAGAMENDA**

**MKOA WA IRINGA**

Simu Na +255 737779767
+255 712 518 989

Sanduku la Posta 1632
IRINGA

Usajiri NECTA S1507

---

Ndugu, Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi……………………………………………………………

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI TAGAMENDA MANISPAA YA IRINGA 2023.**

Ninafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano mwaka……………… Tahasusi ya ……………….

Shule ya Sekondari Tagamenda ipo umbali wa $Km\,2\frac{1}{2}$ kutoka kituo cha mabasi cha Ipogolo kilicho karibu na barabara kuu kwa watokao barabara ya Mbeya au umbali wa Km 5 kutoka stendi Kuu mpya ya Mabasi Igumbilo.

Muhula wa masomo unaanza tarehe 14.08. 2023 hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 13.08. 2023 mwisho wa kuripoti shuleni ni Tarehe 31.08. 2023

**MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**1.0 Sare ya shule**

Zinazo patikana shuleni

a) T –shirt 1 rangi ya kijivu 10,000/=
b) T - shirt 1 rangi ya blue 10,000/=
Jumla 20,000/= aje na pesa taslimu

**1.2 Sare anazotakiwa kuja nazo**

a) Sketi mbili rangi ya khaki rinda box ndefu
b) Sweta 1 rangi ya Blue lenye alama ya V
c) Mashati 2 meupe mikono mirefu
d) Tracksuit 1 rangi ya dark blue

e) Shamba dress sketi rangi ya dark blue rinda box
f) Viatu vyeusi vya ngozi vya kamba visivyo na kisigino.
g) Soksi nyeupe jozi mbili
h) Tai 1rangi ya sketi (khaki).
i) Kwa Waislamu shoti kanzu na Vitambaa viwili (Hijab) visivyo na mapambo yoyote.
j) Jezi bukta na T-shirt (Nyeupe).
k) Raba ya michezo (Nyeupe).

**2.0 MICHANGO**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Fedha hizo zilipwe Kwenye akaunti Namba **60501100063 NMB MKWAWA IRINGA. Jina la akaunti Tagamenda Sekondari.**

*Ni lazima mwanafunzi aje shuleni na stakabadhi halisi ya malipo ya benki (BPS – Bank Pay Slip) iandikwe jina kamili la mwanafunzi na kidato anachosoma. Fedha taslimu haitapokelewa.*

**3.0 MAHITAJI MENGINE MUHIMU**

a) Ream (A4) ya karatasi Mbili (2) kwa Mwaka
b) Godoro la futi 2.5
c) Blanketi 1
d) Mto 1
e) Shuka 2 za pinki na foronya 2.
f) Ndoo 2 za lita 10
g) Picha 02 passportsize za mwanafunzi.
h) Picha za wazazi au walezi (passport size) picha moja kwa kila mzazi/mlezi zibandikwe kwenye fomu iliyoambatanishwa.
i) Chandarua nyeupe futi tatu 1.
j) Jembe 1, Kwanja 1, Reki 1.
k) Mfagio 1 mrefu wa brash wa kufagilia ndani au mfagio wa brush ngumu ya kusugulia sakafu.
l) Vyombo vya chakula, sahani, bakuli, kikombe, na kijiko.
m) Vifaa vya usafi binafsi
n) Vifaa vya masomo kama vile mathematical set, Madaftari makubwa (counter books) kumi na tano na Kamusi ya kingereza.

o) Scientific calculator kwa EGM na HGE.
p) Fedha za matumizi binafsi ya mwanafunzi ya kutosha.

## 4.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 4.1 Sheria na Kanuni za Shule

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
c) Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
i) Kutunza mali za shule;
j) Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
k) Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- *Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;*

- *Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;*

- *Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).*

**4.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

a) Wizi;
b) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
c) Kugoma na kuhamasisha mgomo;
d) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
e) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
f) Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
g) Kufuga ndevu;
h) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
i) Uvutaji wa sigara;
j) Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
k) Kupata ujauzito au kutoa mimba;
l) Kusababisha mimba;
m) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
n) Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
o) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
p) Kudharau Bendera ya Taifa;
q) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
r) Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**5.0 Viambatisho na Fomu Muhimu**

a) Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
b) Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
d) Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**8.0 VITU VISIVYORUHUSIWA SHULENI**

a) Simu za mkononi (charger, line za simu, vocha na vyote vinavyoendana na simu).
b) Pasi za umeme, heater, birika la umeme.
c) Masanduku makubwa hayaruhusiwi kwani hakuna nafasi ya kuyaweka bwenini.
d) Nguo za nyumbani zisizo sare ya shule
e) Hairuhusiwi kufuga nywele, kusuka au kuziweka dawa,
f) Hereni,mikufu, shanga, ufuga na kupakaa kucha rangi, bangili,wanja n.k haviruhusiwi shuleni.
g) Kupeleka chakula bwenini, chakula chochote kiliwe bwaloni na sio vinginevyo.

*N.B Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -*

Mkuu wa shule 0737779767
Makamu Mkuu wa Shule 0764925080
Mwandamizi Taaluma 0756518081
Mwandamizi Malezi 0657653551

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI TAGAMENDA**

**GEOFREY HOSSA**
**MKUU WA SHULE**
**0737779767**

**AHADI YA MZAZI/MLEZI**

Mimi…………………………………………………………………………………………………
Anwani………………………………………………………………………………………………
Simu…………………………………………………………………………………………………
Mzazi/mlezi wa…………………………………………………………………………………

Ninakubali mtoto wangu(Jina)………………………………………………………………
Asome katika shule ya Sekondari Tagamenda kadri alivyopangiwa. Nimempa fedha ya mahitaji inayotakiwa na nitashirikiana na walimu katika suala zima la malezi ya mwanangu na maendeleo ya kitaaluma.

Jina…………………………………………………………………………………………………
Sahihi………………………………………………………………………………………………
Tarehe………………………………………………………………………………………………

Mimi (Jina la mwanafunzi)…………………………………………………………………
Nimeikubali nafasi hii, nitafanya bidii kufuata sheria za shule na kuwatii walezi na jamii kwa ujumla, tena nitafanya bidii kujifunza ili nifaulu vyema masomo yangu.

Jina ………………………………………………………………………………………………
Sahihi………………………………………………………………………………………………
Tarehe………………………………………………………………………………………………

**FORM FOR MEDICAL EXAMINATION**

To be completed by medical officer in respect of all form I entrant's Full name…………………………………………………………………….

Age………………………………years. Sex…………………………….

Blood count (red and white)…………………………………………….

Stool examination…………………………………………………………

Urine analysis……………………………………………………………..

Syphilis test……………………………………………………………….

Eye test…………………………………………………………………….

Ears ………………………………………………………………………….

Chest……………………………………………………………………….

Spleen……………………………………………………………………….

Abdomen…………………………………………………………………

UPT…………………………………………………………………………

**ADDITIONAL INFORMATION,** eg physical or chronicle of family diseases. Etc.

I certify that the above is fit to pursue studies.

Signature…………………………………………………………………

Designation………………………………………………………………………

Section………………………………………………………………………………

Date…………………………………………………………………………………

**TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI**

1. Jina kamili la mwanafunzi...........................................................................
   Utaifa.........................................Dhehebu.................................................
   Mahali alipozaliwa..........................Anuani ya nyumbani............................

2. Jina kamili la baba......................................Kabila..................................
   Dhehebu.........................Simu............................................................
   Kazi.......................................................................................................

3. Jina kamili la mama.....................................................................................
   Kabila...............................................Dhehebu.......................................
   Simu.........................................................................................................
   Kazi............................................................................................

4. Jina kamili la mlezi......................................................................................
   Kabila...............................................Dhehebu.......................................

Simu....................................................Kazi...................................................

5. Je? Wewe unaishi na nani?Jina..........................................
   Uhusiano..........................................................................
   Anuani.....................................................................
   Je? Uliwahi kuwa kiongozi? Ndiyo/Hapana Kama ndiyo taja nafasi ilikuwa ipi...............................................

6. Utakuwa unakwenda wapi wakati wa likizo?....................................
   (Wakati wa likizo unatakiwa kwenda kwa mzazi/mlezi aliyetajwa tu. Kama utabadilisha mahali pa kwenda likizo mzazi/mlezi atoe idhini kwa maandishi mwezi mmoja kabla.

Taja ndugu watatu wanaoweza kuja kukuona shuleni. Bandika picha (passport size) zao hapa chini na uhusiano na mawasiliano yao.

1. Jina.................................................Uhusiano..........................simu .....................................
2. Jina.................................................Uhusiano..........................simu .....................................
3. Jina.................................................Uhusiano..........................simu .....................................

PICHA 1 PICHA 2 PICHA3 PICHA 4

**BAADHI YA VITABU VINAVYOTUMIKA NA WALIMU.**

**HISTORY**

1. Shibital paper one
2. Essential of history paper one by Salehe Yasini
3. Mastering of History paper one by Bakari Madaya
4. Understanding African History Paper one by Joanne's Bigirwamungu
5. Oxford History Paper one and Two form five and six

**ENGLISH**

1. The beautiful ones are not yet born
2. A man of the people
3. An enemy of the people
4. Betrayal in the city

**GEOGRAPHY**

1. The Earth's Physical Environment(4th Edition) By Zist Kamili
2. MSABILA D.T(2010) A comprehensive approach to physical geography)
3. Essentials of Physical (eight edition) by Robert E.Gabher
4. Zisti kamili (2016) Practical Geography.
5. Msabila D.T (2010) An Intergrated Regional study on Human and Economic Geography Advanced level paper 2.
6. Geography an integrated approach fourth edition by (David Waugh 2014)

**KISWAHILI**

1. Nadhalia ya lugha Kiswahili 1 kidato cha tano na sita mwandishi Nyambari Nyangwine na Masebo J.A
2. Sarufi maumbo ya Kiswahili SANIFU (SAMAKISA) sekondari na vyuo by Kihore na wenzake
3. Nadharia ya Fasihi kidato cha tano na sita by Nyambari Nyamnwine
4. Tahakiki ya vitabu teule kidato cha tano na sita by Nyambari Nyangwine
5. Vitabu vya ushairi (chungu tamu fungute ya uhuru,Kimbungu)
6. Riwaya (mfadhili, usiku utakapokwisha, vuta nikuvute)
7. Tamthilia (ngunzo mama, morani kivuli kinaishi)

**ECOMOMICS**

1. Simplified Economics by N.A Saleem (New Edition)
2. Essentials for A-level Economics by Ambros Odhimbo
3. Advanced level Economics paper 1 by Ambilikile C.M
4. Advanced level Economics paper 2 by Ambilikile C.M
5. Principles of Economics by Jhingan, M.J
6. Managerial Economics by H.L Ahuja(New Edition

**ADVANCE MATHEMATICS**

1. Conceptual Advanced mathematics (Form 5 & 6) by P. L Mayombya
2. Essential for A level Pure Mathematics Form 5 & 6 by Telemu Majigwa
3. Pure mathematics 1 and 2 S. K Backhouse